# KASSU JET MOCK 2024

**102/3**

# KISWAHILI

**KARATASI YA 3**

**FASIHI**

**MUDA: SAA 2½**

**JINA……………………………………………………………………………………**

**SHULE………………………………………………… SAHIHI……………………**

**NAMBARI YA USAJILI……………………………… MKONDO……………………**

*Cheti cha Kuhitimu Kisomo cha Sekondari (KCSE)*

**Maagizo**

***(a)*** *Andika jina lako na nambari yako ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.*
***(b)*** *Tia sahihi yako kisha uandike tarehe ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.*
***(c)*** *Jibu maswali* ***manne*** *pekee.*
***(d)*** *Swali la kwanza ni la* ***lazima.***
***(e)*** *Maswali hayo mengine matatu yachaguliwe kutoka sehemu nne zilizobaki;yaani:Riwaya, Tamthilia,,Hadithi Fupi na Ushairi.*
***(f)*** *Usijibu maswali* ***mawili*** *kutoka sehemu moja.*

**Kwa Matumizi ya Mtahini Pekee**

| Swali | Upeo | Alama |
|---|---|---|
| 1 | 20 | |
| | 20 | |
| | 20 | |
| | 20 | |
| | | |

## SEHEMU A: HADITHI FUPI (LAZIMA)

**D.W. Lutomia na Phibbian Muthama : Mapambazuko Ya Machweo Na Hadithi Nyingin**

**Lazima**

Athari ya mawazo yake ilijiandika dhahiri shahiri usoni mwake. Alianza kwa kuachia tabasamu pana mithili ya msafiri aliyefika salama. Baada ya dakika chache, machozi yalianza kumtoka njia mbilimbili huku kajishika tama. Alifikiria kuhusu mtihani uliodhamiriwa kuanza siku ya Jumanne. Mtihani ambao ungemwezesha kupata ufadhili katika shule ya upili ya bweni ikiwa angepita vyema. Hili ndilo wazo lililozua tabasamu. Lakini, angefeli je? Hatima yake ingekuwa ipi? Maswali haya yalimliza yakamwacha akisinasina kama mgonjwa wa mafua. Akiwa katika hali hii, aliyakumbuka maneno ya mwalimu mkuu, "Mizizi ya elimu ni michungu ila matunda yake ni matamu. Ikiwa mnataka kuyaonja matunda ya elimu, lazima mtie bidii kwani mtaka cha mvunguni sharti ainame."

Akiwa amezama kwenye lindi la mawazo, alizinduliwa na sauti ya Yunuke ikimwita, "Sabina! Sabina! Sabinaa!"

Changanua mtindo kwenye kifungu. **(alama 8)**

Suala la kazi na bidi limeangaziwa kwa kina kwenye diwani ya mapambazuko ya machweo. Tetea ukweli wa kauli hii kwa kurejelea hadithi zifuatazo:

Fadhila za punda

Mapambazuko ya machweo

Sabina **(alama 12)**

## SEHEMU B: RIWAYA

**Clara Momanyi:** Nguu za Jadi.

Jibu swali la 2 au la 3

**2.** **"***atawatoa wananchi wa Matuo kutoka katika mchanga wa moto unaowaunguza."*

**a)** Weka dondoo hili katika muktadha wake_ **(aL4)**

**b)** Tambua mbinu ya uandishi katika dondoo hili. **(aL2)**

**c)** Kwa kurejelea riwaya nzima, Fafanua jinsi wahusika mbalimbali wanaunguzwa naserikali **(aL14)**

**3.** Eleza jinsi Mtemi Lesulia amejenga usaliti katika riwaya ya Nguu za Jadi. **(aL20)**

## SEHEMU C: TAMTHILIA

**Timothy Arege:** Bembea Ya Maisha

Jibu swali la 4 au la 5

**4.** "Hata nikiitwa nitaondoka nikiwa nimeridhika."

a)Eleza muktadha wa dondoo hili . **(alama 4)**

b)Kwa hoja **tano**, eleza sifa za msemaji wa maneno haya . **(alama 5)**

c)Tambua mbinu **moja** ya lugha iliyotumika katika dondoo hili. **(alama 1)**

d) Wahusika mbalimbali kwenye tamthilia wamekubwa **na majonzi na furaha**. Thibitisha. **(alama 10)**

**5.** "...Tayari unakuwa umeonja seli.Hata wahudumu wenyewe hawana mlahaka mwema .amri na vitisho kama askari.Unashindwa kama uuguze moyo ama ugonjwa.Katika wodi hewa iliyojaaa harufu ya dawa imezagaa,vitanda vimesalimu amri mpaka shiti zikagura.Yaani hali nzima haikupi matumaini ya kutoka ukiwa bora.matumaini yanadidimia .Tumaini lako unaliweka katika sala. "

**(a)** Tambua toni mbili katika kifungu **hiki** **(alama 2)**

**(b)** Tambua aina mbili za taswira katika dondoo hili **(alama 2)**

**(c)**Kando na taswira chambua vipengele vingine vya kimtindo **(alama 6)**

**(d)** Fafanua namna mandhari ya dondoo hili yalivyochangia kujenga tamthilia ya Bembea ya Maisha. **(alama 10)**

## SEHEMU D: USHAIRI.

*Jibu swali la 6 au la 7*

***<u>6. Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali</u>***

**<u>Taifa ni Ushuru</u>**

Lau kama ingakuwa, madhali tuna uhuru
Watu kodi kutotowa, na kuifanya kufuru
Vipi nchi ingakuwa, taifa bila ndururu
Taifa halingakuwa, bilashi bila ushuru

Hivi taifa kumea , nakuendelea mbele
Kwamba lajitegemea, haliwategei wale
Yataka kujitolea, ushuru bila kelele
Taifa halingakuwa, bilashi bila ushuru

Wafanyikazi wa umma, mfano mwema walimu
Wauguzi mahashuma, daktari wahadimu
Bila hizi darahima, vipi wangalihudumu?
Taifa halingakuwa, bilashi bila ushuru

Si vyema kuombaomba, kwa wageni kila mara
Huwa twajifunga Kamba, na kujitia izara
Adha zinapotukumba, kujitegemea bora
Taifa halingakuwa,bilashi bila ushuru

Miradi ya maendeleo, yahitaji darahima
Ndo tufikie upeo, ulio dunia nzima
Wadogo na wenye vyeo, bila kodi tutakwama
Taifa halingakuwa, bilashi bila ushuru

Ushuru si kwa wanyonge, wasokuwa na uwezo
Watozwe hata wabunge, na wengine wenye nazo
Yeyote asijitenge, kodi akalipa bezo
Taifa halingakuwa, bilashi bila ushuru

Kwetu kutoa ushuru,ndiko kujitegemea
Pasiwepo na udhuru, usio wa kuelea
Huwa ni kama kiguru, asenao kutembea
Taifa halingakuwa, bilashi bila ushuru

**Maswali**

**(a)**Tambua hadhira inayolengwa katika shairi hili. **(alama 1)**

b)Huku ukitoa mfano,onyesha mbinu **tatu** ambazo mshairi ametumia kutosheleza uhuru wake. **(alama 3)**

c)Bainisha aina **tatu** za urudiaji zinazojitokeza katika utungo huu. **(alama 3)**

d)Eleza muundo wa ubeti wa sita. **(alama 4)**

e)Andika ubeti wa **nne** katika lugha ya nathari/tutumbi **(alama 4)**

f)Kwa kutolea mfano,taja mbinu **tatu** za kimtindo zilizotumika katika shairi hili. **(alama 3)**

g)Weka shairi hili katika bahari yake ukirejelea : **(alama 2)**

i)Vipande

ii)Vina

**7. Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali**

Sikilizeni wimbo huu:
Niliokuwa mtoto nilitwa chacha Kwa matamshi yangu ya sasa
Nilipokuwa mtu mzima niliitwa Manywele Nilipokuwa mwalimu nikaitwa Bure.

Huu utakuwa wimbo wako Utakapostaafu urudipo nyumbani Umelewa kangara na nyayo zako
Zikishindwa kulenga njia nyembamba vijijini. Utakuwa kichekesho cha watoto Watakaoukuita, Ticha! Popote upitapo.

Kumbuka mwalimu utakapostaafu, Mijusi watataga mayai ndani ya viatu Vyako vilivyokwisha visiginino.
Na ndani ya sidiria chakavu Zilizoshikizwa Kamba kwa pini
Mende watazaliana ndani ya chupa tupu Za marashi na za bia.

Na manyigu yatajenga ndani ya kofia Zilizosahaulika kutani

Utakapokufa nge watazaliana Chini ya jiwe juu ya kaburi lako, Na mlevi fulani akipita atapenga

Na kupangusa vidole kwenye jiwe pweke

Mwanzo na mwisho wako ndio huo.

Lakini wakati ungali hai

Unaweza kubadilisha mkondo wa maji Lakini kwanza mzungumze. Wewe na mimi. Acha mioyo yote izungumzwe

Baada ya kunyanyaswa Na kisha nusu mshahara.

Utafundisha tena nyimbo kuwasifu viongozi? Utafundisha tena ngonjera?

Utapeleka tena wanafunzi asubuhi Wakajipange barabarani kusubiri Mgeni afikaye saa kumi na apitapo

Apunga tu mkono kuwatia kichaa cha shangwe

Na huku nyuma mwasambaa na njaa?

Tazama hilo runda madaftari mezani Utalimaliza kwa mshahara mkia wa mbuzi? Tuzungumze. Ninyi na mimi.

Acha mioyo yetu izungumze

Mkiwa waoga na kujikunja kama jongoo Mtawekwa kwenye vijiti na kutupwa Nje ya ua, ndani mtawaacha

Wacheza ngoma wakitunga nyimbo mpya

Sikilizeni walimu,

Anzeni kufundisha hesabu mpya

Mjinga mmoja kujumlisha na wezi ishirini Ni sawa na sifuri. Hapana utawala Fundisheni historia historia mpya

Hapo zamani za sasa Hapakuwa na serikali.

Sikilizeni kwa makini Umoja hatuna

Twasambaratika kama nyumba Tulicho nacho ni woga,

Na kinachotuangusha ni unafiki. Lakini tusikate tamaa kama mbuni. Tukiupata umoja bado tunayo silaha. Kura.

**<u>Maswali</u>**

Fafanua sifa za shairi huru zinazojitokeza katika shairi hili. **(al. 5)**

Eleza jinsi maudhui ya utamaushi yanavyojitokeza ukimrejelea nafsi-nenewa**.** **(al. 4)**

Nafsi-nenewa anapaswa kujilaumu kwa masaibu yake. Thibitisha**.** **(al. 2)**

(i) Bainisha nafsi-neni katika shairi hil**i.** **(al. 1)**

Taja toni ya shairi hili. Toa mfano. **(al. 2)**

Eleza matumizi mawili mawili ya usambamba na jazanda katika shiri hili. **(al. 4)**

Eleza maana ya kufungu kifuatacho:

Mjinga mmoja kujumlisha na wezi ishirini ni sawa na sufuri. **(al. 2)**

**SEHEMU E: FASIHI SIMULIZI**

8. **Soma utungo ufuatao kisha ujibu maswali**

**1.** Angole angole mwanangu

Mwanangu nakuchombeza

Nakuchombeza ulale

Ulale ukiamka

Nikupikie ubwabwa

Na mchuzi wa papa

Ukilia waniliza, wanikumbusha

Ukiwa wa baba na mama

**2.** Baba na mama watende

Ilimu kunikatizia

Ng'ombe, mbuzi kupokea

Kunioza dumu kongwe

Haliuki na halende

Kazi kupiga matonge

**3.** Likingia mvunguni

Lavunjavunja vikombe

Likilala kitandani

Languruma kama gombe

a) Bainisha kipera cha utungo huu. Thibitisha. **(alama 2)**

b) Eleza ujumbe unaofumbwa katika wimbo huu. **(alama 5)**

c) Tambua mbinu za kifani ambazo zimetumiwa kuwasilisha utungo huu. **(alama 3)**

d) Bainisha shughuli mojamoja ya kijamii na ya kiuchumi ambazo huendelezwa katika jamii ya utungo huu. **(alama 2)**

e) Unakusudia kukusanya data kuhusu kipera hiki. Eleza manufaa manne ya kutumia mahojiano. **(alama 4)**

f) Kipera hiki kinazidi kufifia katika jamii yako. Fafanua njia nne ambazo jamii ya kisasa inaweza kutumia kukuza na kuendeleza kipera hiki. **(alama 4)**